ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

*2022/23*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2023**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

*2022/23*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2023**

## Utangulizi

Tamko la Sera ya Fedha lililotolewa na Benki Kuu mwezi Juni 2022, lilibainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2022/23, katika kuhakikisha utulivu wa bei huku ikichagiza ukuaji endelevu wa uchumi. Taarifa hii ya mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2022/23, inatoa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23. Vilevile, taarifa hii inatoa mwelekeo wa uchumi wa Tanzania, pamoja na sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2022/23, inayolenga mfumuko mdogo wa bei, pamoja na kusaidia kukuza uchumi.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Mwaka 2022 uchumi wa dunia ulikabiliwa na changamoto zilizoambatana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi uliosababishwa na vita nchini Ukraine, kuibuka kwa maambukizi mapya ya UVIKO-19, pamoja na mabadiliko ya tabia nchi. Kutokana na mwenendo huo, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kupungua, ambapo kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) na Benki ya Dunia, mwaka 2022 uchumi wa dunia unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.4 na asilimia 2.9, mtawalia. Aidha, uchumi kwa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.8. Kutokana na matarajio ya kuendelea kupungua kwa shughuli za kiuchumi katika nchi zilizoendelea, na athari za vita nchini Ukraine, pamoja na kupanda kwa viwango vya riba za

mikopo katika soko la dunia, IMF imekadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kushuka hadi asilimia 2.9 kwa mwaka 2023. Hali kadhalika, Benki ya Dunia inakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia wa asilimia 1.7 mwaka 2023.

Mfumuko wa bei ulikuwa juu ya malengo, hususan katika nchi zilizoendelea kiuchumi katika mwaka 2022. Hata hivyo kufuatia kupungua kwa changamoto za mvurugiko wa mnyororo wa ugavi na kushuka kwa baadhi ya bei za bidhaa, pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza mfumuko wa bei katika nchi nyingi, kasi ya mfumuko wa bei imeanza kupungua. Vilevile, mfumuko wa bei ulikuwa juu ya kigezo cha mtangamano wa uchumi katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wa kiwango kisichozidi asilimia nane (8), isipokuwa Tanzania. Hali hii imeonekana pia katika ukanda wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ambapo mfumuko wa bei katika nchi hizi ulikuwa juu ya wigo wa mtangamano wa kiuchumi wa asilimia 3 hadi 7, isipokuwa kwa Tanzania, Shelisheli, Eswatini na Namibia. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei ilianza kupungua kuelekea mwishoni mwa mwaka 2022, kutokana na kushuka kwa bei za nishati duniani, pamoja na kupungua kwa baadhi ya changamoto katika mnyororo wa ugavi. Mwenendo huu unatarajiwa kuendelea katika mwaka 2023, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza mfumuko wa bei kupitia benki kuu za nchi nyingi duniani.

Katika nusu ya pili ya mwaka 2022, bei za bidhaa katika soko la dunia ziliendelea kuwa juu, japokuwa dalili za kupungua zimeanza kuonekana. Mathalani, bei ya mafuta ghafi ya nishati ilipungua hadi wastani wa dola za Kimarekani 78.1 kwa pipa mwezi Desemba 2022, kutoka dola 105.1 kwa pipa mwezi Julai 2022, kutokana na kupungua kwa mahitaji kulikosababishwa na matarajio ya mdororo wa kiuchumi katika nchi zilizoendelea na kusimamishwa mara kwa mara kwa shughuli za kiuchumi (*lockdown*) katika nchi ya China. Bei za mbolea zimeendelea kushuka kutokana na kupunguza matumizi, kulikosababishwa na gharama kubwa ya pembejeo hiyo na kupatikana kwa mbolea mbadala katika nchi mbalimbali. Kwa upande wa mazao, bei ya kahawa, ngano na chai zilipungua. Kupungua kwa bei ya ngano kulitokana na makubaliano ya Umoja wa Mataifa ya kuruhusu usafirishaji wa ngano kutoka nchini Ukraine. Aidha, bei ya mafuta ya kula iliongezeka kutokana na ongezeko la mahitaji, wakati bei ya dhahabu iliongezeka kutokana na kushuka kwa thamani ya dola ya Marekani, baada ya Benki Kuu ya Marekani (*The Federal Reserve*) kupunguza kasi ya ongezeko la riba yake.

**Utekelezaji wa Sera ya Fedha Katika Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2022/23**

Utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2022/23, ulilenga kusaidia kufikiwa kwa malengo mapana ya kiuchumi ya Serikali ambayo ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 na mfumuko wa bei wa asilimia 5.4. Ili kusaidia kufikiwa kwa malengo haya, Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kutekeleza sera ya

fedha yenye malengo yafuatayo:

i. ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 11.4;

ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.3;

iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.7; na

iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, Benki Kuu ya Tanzania ilitekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kiwango cha ongezeko la ukwasi katika uchumi, ili kuhakikisha utulivu wa bei na kuchochea kuimarika kwa shughuli mbalimbali za uchumi baada ya janga la UVIKO-19 na athari za vita nchini Ukraine. Utekelezaji huu wa sera ya fedha ulifanikiwa kudumisha kiwango cha kutosha cha ukwasi katika uchumi, hali ambayo imesaidia kuweka mazingira ya kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kusaidia kufikiwa kwa vigezo vya makubaliano ya programu ya IMF kwa Tanzania chini ya mpango wa *Extended Credit Facility (ECF).*

Hata hivyo, utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, ulikabiliwa na changamoto ya ongezeko la bei za nishati na bidhaa nyingine katika soko la dunia, hususan mafuta ya kula, ngano na mbolea. Vilevile, kuchelewa kwa mvua za vuli katika baadhi ya maeneo nchini kulisababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na kusababisha ongezeko la bei. Aidha,

uhaba wa chakula katika nchi jirani ulichangia kuongezeka kwa bei za vyakula nchini. Ili kudhibiti kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei nchini, Benki Kuu ilipunguza kwa tahadhari kiwango cha ongezeko la ukwasi kwenye uchumi, hali ambayo iliendelea kuimarisha ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Sera hii ilitekelezwa kwa kutumia nyenzo mbalimbali kama vile kuingia mikataba ya mauziano ya dhamana za Serikali kwa muda mfupi (*repurchase agreements*) na kwa kuuza dhamana maalum za Serikali kwa lengo la kupunguza ukwasi kwenye uchumi (*liquidity papers*).

Kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki ilipungua hadi wastani wa asilimia 3.59 katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2022, kutoka asilimia 3.85 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Wastani wa ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulikua kwa asilimia 11.8, sanjari na lengo la asilimia 10.3 kwa mwaka 2022/23, wakati ukuaji wa fedha taslimu (*reserve money*) na mikopo kwa sekta binafsi ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 16.3 na asilimia 21.9, mtawalia. Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kilikuwa juu ya lengo lililowekwa la asilimia 10.7 kwa mwaka 2022/23. Ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa uhitaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kufuatia uwekezaji unaotekelezwa na Serikali kwenye miundombinu, uboreshwaji wa mazingira ya kufanya biashara, na sera wezeshi za kibajeti zinazoendelea kuchochea kuongezeka kwa shughuli binafsi za kiuchumi nchini.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

***Tanzania Bara***

Uchumi umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha, pamoja na changamoto zitokanazo na misukosuko ya kiuchumi duniani, iliyosabishwa na vita nchini Ukraine na athari za UVIKO-19 kwa baadhi ya nchi washirika wa biashara. Katika robo tatu za kwanza za mwaka 2022, uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2, ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi na uzalishaji viwandani. Kwa mujibu wa viashiria vya awali, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.5 au zaidi katika robo ya nne ya mwaka 2022, na hivyo kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa kuvuka lengo la ukuaji wa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022.

Mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.8 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, ikilinganishwa na asilimia 4.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ongezeko hili lilichangiwa na kupanda kwa bei za vyakula na mafuta ya nishati. Aidha, pamoja na ongezeko hilo, mfumuko wa bei umeendelea kubakia ndani ya lengo la nchi la asilimia 5.4, na vigezo vya mtangamano vya nchi wanachama wa EAC na SADC.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, ujazi wa fedha ulikua kwa wastani wa asilimia 11.8 sanjari na lengo la asilimia 10.3 kwa mwaka 2022/23. Wastani wa ukuaji wa fedha taslimu (M0) ulikuwa ni asilimia 16.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 11.4, hali

iliyotokana na ongezeko la matumizi ya Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo, pamoja na kuongezeka kwa uhitaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kuongezeka na kuchochea ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kufikia wastani wa asilimia 21.9, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.7 kwa mwaka 2022/23. Kasi hii kubwa ya ukuaji ambayo haijawahi kufikiwa kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita ilichangiwa na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi, pamoja na mikopo maalumu iliyotolewa na Benki Kuu kwa benki za biashara ili ziweze kukopesha wawekezaji kwenye shughuli za kilimo kwa riba nafuu. Pia, ongezeko hili lilichochewa na hatua zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbolea na mafuta ya nishati (petroli, dizeli na mafuta ya taa), punguzo la kodi katika uzalishaji wa mafuta ya kula, ongezeko la bajeti kwa wizara ya kilimo na hatua zinazoendelea kutekelezwa na Serikali katika jitihada za kuboresha mazingira ya kibiashara nchini, hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi katika sekta binafsi.

Shughuli zilizokuwa na ukuaji mkubwa wa mikopo ni kilimo (asimilia 46.1), shughuli binafsi za kiuchumi (asilimia 28.8), viwanda (asilimia 28.3) na biashara (asilimia 24.6). Ongezeko kubwa la mikopo kwa sekta ya kilimo, limechangiwa na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ili kuchochea ukuaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi zinazojishughulisha na kilimo, pamoja na jitihada za Serikali katika kukuza sekta ya kilimo nchini. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuimarika zaidi katika nusu ya pili ya mwaka 2022/23, kufuatia utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, na kuendelea

kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na maboresho katika mazingira ya biashara.

Viwango vya riba za mikopo inayotolewa na benki havikuwa na mabadiliko makubwa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23. Wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 16.09, ukilinganishwa na asilimia 16.55 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, wastani wa riba za amana uliongezeka na kufikia asilimia 7.34, kutoka asilimia 6.74 kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kasi ndogo ya kupungua kwa riba za mikopo inaashiria uhitaji wa kuendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha, ambapo  Benki Kuu imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kufanya maboresho zaidi yatakayopelekea kuendelea kupungua kwa riba za mikopo na kuongeza tija katika uzalishaji mali nchini.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,318.33 kwa dola ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,308.30 kwa dola ya Marekani katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hii ilikuwa ni sawa na kupungua kwa thamani ya shilingi kwa wastani wa chini ya asilimia moja, hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, mfumuko mdogo wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wa kibiashara, na nakisi ndogo ya urari wa bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje. Hali hii pia ilichangiwa na hatua zilizochukuliwa katika kuongeza uwazi na utulivu katika soko la fedha za kigeni nchini.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali ulikuwa sanjari na malengo yaliyopangwa katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, licha ya changamoto zilizotokana na misukosuko ya kiuchumi duniani. Mapato ya ndani (mapato ya kodi na yasiyo ya kodi) yalikuwa shilingi bilioni 13,414.1, sawa na asilimia 96.7 ya malengo. Matokeo haya yamechangiwa na kuimarika kwa usimamizi wa ukusanyaji mapato, sambamba na ongezeko la matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji mapato. Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 16,261.6, ambapo shilingi bilioni 7,076 zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo na kiwango kilichobakia kilitumika kwenye matumizi ya kawaida.

Deni la taifa limeendelea kuwa himilivu, huku thamani ya deni la Serikali kwa sasa ikiwa asilimia 32.5 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55. Hadi mwishoni mwa mwezi Desemba 2022, deni la ndani na nje la Serikali lilifikia dola za Marekani milioni 32,358 ikiwa ni ongezeko la dola za Marekani milioni 1,466.4 kutoka kiwango kilichorekodiwa mwezi Juni 2022. Mikopo hii ilielekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo ya uchumi wa nchi.

Sekta ya nje imeendelea kuwa imara licha ya athari zitokanazo na misukosuko katika uchumi wa dunia. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ilikuwa dola za Marekani milioni 3,084.2, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,123.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22, kutokana na ongezeko la gharama ya

uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kufuatia kupanda kwa bei za bidhaa. Aidha, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa katika viwango toshelezi, kufikia dola za Marekani milioni 5,177.2 mwezi Desemba 2022, kiasi ambacho kinatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa miezi 4.7. Kiwango hiki ni ndani ya lengo la nchi la miezi isiyopungua minne na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza angalau miezi minne na nusu. Kiwango cha akiba kinatarajiwa kuongezeka kutokana na kuendelea kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 17.4, kufikia dola za Marekani milioni 6,644.5, kufuatia ongezeko la mapato ya usafirishaji, bidhaa asilia, madini na bidhaa za viwandani. Wakati huohuo, mapato yatokanayo na huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 2,663.4, ikiwa ni ongezeko la asilimia 47.4, kutokana na kuimarika kwa shughuli za utalii na uchukuzi. Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 60.6 kufikia 879,523. Kufuatia mwenendo huu, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje inatarajiwa kufikia asilimia 5 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2022/23, ikilinganishwa na asilimia 4.6 katika mwaka 2021/22, hali inayoakisi ongezeko la gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa hususan mafuta ya nishati na vyakula.

Sekta ya benki imeendelea kuwa thabiti, yenye mtaji na ukwasi wa kutosha, ikiendelea kutengeneza faida kwa kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23. Amana na rasilimali ziliendelea kuongezeka kuendana na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma. Wakati huohuo, ubora wa rasilimali za mabenki uliendelea kuongezeka, ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua kutoka asilimia 7.8 mwezi Juni 2022 hadi kufikia asilimia 5.8 mwezi Desemba 2022, ukikaribia kiwango kinachokubalika cha chini ya asilimia 5, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 13 mwaka 2017. Kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu ni moja kati ya mafanikio makubwa ya Benki Kuu ya Tanzania, hali ambayo inatarajiwa kuongeza kasi ya ukuaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji uchumi. Aidha, Benki Kuu imeendelea kufanya jitihada za kupunguza kiwango cha mikopo chechefu ili kiweze kufikia chini ya asilimia 5. Hatua hizi ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa na sekta ya benki katika kupunguza kiwango cha mikopo chechefu, kuhimiza mabenki kuongeza umakini katika kuidhinisha mikopo kwa kufuata miongozo iliyopo pamoja na kuzitaka benki kuwasilisha na kutumia taarifa za wakopaji kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji. Vilevile, Benki Kuu inaendelea kuhimiza wafanyakazi kufuata maadili na miongozo ya kiutendaji iliyoainishwa na Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA).

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi, sanjari na kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kufanya miamala, hali iliyochangiwa na ongezeko la matumizi ya

simu za mkononi katika kupata huduma za fedha. Matumizi ya simu za mkononi yamekuwa kichocheo kikubwa katika kuongeza huduma jumuishi za fedha nchini. Aidha, Benki Kuu imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Mfumo wa Malipo ya Papo Hapo (Tanzania Instant Payment System (TIPS)), ambao utarahisisha malipo madogomadogo kwa usalama na ufanisi baina ya watoa huduma za fedha kupitia mitandao ya kidigitali. Mfumo huu unatarajiwa kupunguza gharama za malipo na kuboresha matumizi ya mfumo rasmi wa sekta ya fedha.

**Zanzibar**

Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika na kukua kwa wastani wa asilimia 5.3 katika kipindi cha robo tatu za mwaka 2022, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2022. Ukuaji huu ulitokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathirika na janga la UVIKO-19. Ukuaji huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli zitokanazo na huduma ya malazi na chakula, mifugo, ujenzi na uzalishaji viwandani. Aidha, ukuaji unatarajiwa kuendelea kuwa juu katika robo ya mwisho ya mwaka 2022, na kipindi chote cha mwaka 2023, kutokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayoendelea, pamoja na kuimarika kwa shughuli zinazohusiana na utalii.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 6.7, kutoka asilimia 2.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22, kutokana na ongezeko la bei za

bidhaa za vyakula. Mfumuko wa bei za vyakula uliongezeka hadi kufikia asilimia 9.4 kutoka asilimia 0.2, kutokana na kuongezeka kwa bei za mazao hususan mahindi, mchele wa Mbeya na unga wa ngano. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la tarakimu moja katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2022/23, pamoja na changamoto zitokanazo na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23, mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yaliongezeka kwa asimilia 41.6 na kufikia shilingi bilioni 599.3, kutoka kiasi kilichokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 582.7, sawa na asilimia 97.1 ya lengo na kiasi kilichobaki kikiwa ni misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 516.5, sawa na asilimia 99.8 ya lengo. Ukusanyaji wa mapato unaendana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi pamoja na usimamizi thabiti katika ukusanyaji wa mapato. Wakati huohuo, matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 687.8, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 487.1, na kiasi kilichobaki kikiwa kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 2,700.1 mwezi Desemba 2022, kutoka shilingi bilioni 1,224 mwishoni mwa mwezi Juni 2022, ambapo deni la nje lilikuwa ni asilimia 88.2. Ongezeko la deni la Serikali limetokana na  mikopo mipya, marekebisho yaliyoambatana na uhakiki wa takwimu za madeni na kushuka kwa thamani ya shilingi.

Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 187.3, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 89.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ongezeko hili liliakisi kupanda kwa gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kufuatia ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, pamoja na kupungua kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalipungua kutoka dola za Marekani milioni 120.9 hadi dola za Marekani milioni 114.5. Aidha, mapato yatokanayo na uuzaji wa huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 9.5, kufikia dola za Marekani milioni 64.7. Thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 37.7, na kufikia dola za Marekani milioni 308.0, hali iliyochangiwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa za nishati, chakula, mashine na vifaa vya ujenzi.

**Mwelekeo wa Uchumi**

Misukosuko katika uchumi wa dunia imeendelea kudhoofisha shughuli za kiuchumi na hivyo kuchangia ongezeko la mfumuko wa bei nchini. Vita inayoendelea nchini Ukraine itaendelea kuathiri shughuli za kiuchumi na kuchangia ongezeko la mfumuko wa bei katika nusu ya pili ya mwaka 2022/23, japo athari zinatarajiwa kupungua ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Hali hii inatokana na kupungua kwa vikwazo katika mnyororo wa ugavi na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Vilevile, kuimarika kwa shughuli za uzalishaji ndani ya nchi, hususan mazao ya chakula,

kunatarajiwa kupunguza kasi ya mfumuko wa bei na kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa. Kutokana na matarajio hayo, ukuaji wa Pato la Taifa kwa Tanzania Bara unatarajiwa kuwa asilimia 5.3 mwaka 2023, kutokana na ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kurejea kwa shughuli za utalii na uwekezaji wa Serikali kwenye sekta za uzalishaji na miradi ya kimkakati. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.1 mwaka 2023, kufuatia kurejea kwa shughuli za uchumi wa bluu na utalii. Vilevile, utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti, pamoja na maboresho yanayofanyika katika mazingira ya kufanya biashara, yanatarajiwa kuchangia katika ukuaji endelevu wa uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya tarakimu moja katika nusu ya pili ya mwaka 2022/23, sawia na lengo la asilimia 5.4 na asilimia 5 kwa Tanzania Bara na Zanzibar, mtawalia. Hali hii itachangiwa na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, na utulivu wa thamani ya shilingi.

Sekta ya fedha inatarajiwa kuendelea kuwa imara na kuchochea ukuaji wa uchumi, kutokana na usimamizi thabiti wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya udhibiti katika kusimamia sera na misingi ya kanuni za uendeshaji. Hatua hizi zitahusisha pia kuboresha sera na mifumo ya udhibiti, usimamizi unaozingatia viashiria vya hatari (*risk based supervision*), na kuilinda sekta ya fedha dhidi ya misukosuko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, hatua za kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini na

kupungua kwa mikopo chechefu kutachangia kuongezeka kwa faida na ukuaji wa sekta ya fedha. Vilevile, ubunifu unaoendelea katika utoaji wa huduma za fedha unatarajiwa kuongeza kiwango cha huduma jumuishi za fedha na hivyo kuwezesha utekelezaji wa sera ya fedha na utoaji wa mikopo mingi zaidi kwa sekta binafsi.

Katika maandalizi ya kuhamia katika mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba (*interest based monetary policy framework*), Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuboresha mfumo unaotumika kufanya maoteo ya viashiria mbalimbali vya kiuchumi na kuweka miundombinu wezeshi ya masoko ya fedha. Aidha, shughuli nyingine zinazotarajiwa kufanyika katika kipindi kilichosalia cha mwaka 2022/23 ni pamoja na kuandaa miongozo ya utekelezaji wa sera ya fedha inayotumia riba, sambamba na kutoa elimu kwa wadau kuhusu mfumo huo mpya.

## Hitimisho

Shughuli za kiuchumi duniani zinatarajiwa kuendelea kuathirika kiasi, japo dalili za kuimarika zimeanza kuonekana. Changamoto zinazotokana na athari za UVIKO-19 pamoja na vita nchini Ukraine zimeendelea kupungua. Mfumuko wa bei ambao ulikuwa juu zaidi ya malengo ya benki kuu katika nchi nyingi zilizoendelea, umeanza kupungua. Mabadiliko haya yenye matumaini yanatarajiwa kuimarisha shughuli za uzalishaji nchini na kusaidia kupungua kwa mfumuko wa bei. Vilevile, matarajio ya kuimarika kwa shughuli za kiuchumi yatachangiwa pia na utekelezaji wa sera madhubuti za kiuchumi, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara, ujenzi wa miundombinu na ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Tanzania Bara na Zanzibar unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.3 na asilimia 6.1 mwaka 2023, mtawalia. Kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kupungua na kubakia ndani ya tarakimu moja katika nusu ya pili ya mwaka 2022/23, sambamba na lengo la asilimia 5.4 kwa Tanzania Bara na asilimia 5.0 kwa Zanzibar, kutokana na matarajio ya ongezeko la uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini kufuatia kurejea kwa hali nzuri ya hewa na kuendelea kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Kutokana na matarajio ya mwenendo wa uchumi, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kiwango cha ongezeko la ukwasi kwenye uchumi katika nusu ya pili ya mwaka 2022/23. Hatua hii ya kisera itasaidia kudhibiti

shinikizo kwenye mfumuko wa bei linalotokana na misukosuko katika uchumi duniani bila kuathiri kasi ya kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Ili kufikia malengo haya, Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo mbalimbali za utekelezaji wa sera ya fedha katika kutimiza jukumu hili la msingi, huku ikihakikisha utulivu wa soko la fedha. Msimamo huu wa sera ya fedha unalenga pia kufikiwa kwa malengo ya programu ya Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) kupitia mpango wa *Extended Credit Facility* (*ECF*). Aidha, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo mzima wa uchumi wa dunia kwa lengo la kuchukua hatua za ziada za kisera endapo zitahitajika ili kuhakikisha utulivu wa uchumi. Kwa muktadha huu, Benki Kuu ya Tanzania inatarajia kuwa malengo yaliyoainishwa katika Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2022/23 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Barabara ya Jakaya Kikwete 40184,
S.L.P 2302, Dodoma, Tanzania
Baruapepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: http://www.bot.go.tz